**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/472/LZ/2024/11**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000015**

**KATI YA**

**SOCCER DOMICIAN KACHELE ....................................................... MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MWANZA (MWAUWASA) ........................................... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 14 mwezi Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 14 mwezi Februari 2025 kwa madai kwamba Mlalamikiwa aamriwe kupeleka huduma ya maji nyumbani kwa Mlalamikaji Kabohoro jijini Mwanza haraka iwezekanavyo.

Mlalamikaji anadai kwamba mnamo tarehe 15 Novemba 2024, alilipia huduma ya maji ofisini kwa Mlalamikiwa kiasi cha TZS 222,826.20 lakini mpaka analeta shauri lake EWURA, imepita mwezi mmoja bado hajapatiwa huduma hiyo. Hivyo ameamua kuleta malalamiko yake kwa Mamlaka kwa hatua zaidi.

Baada ya kupokea malalamiko hayo mnamo tarehe 15 Novemba 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Pamoja na kumuandikia wito wa kuwasilisha utetezi, EWURA iliwasiliana na Mlalamikiwa ili kuona kama ataweza kutatua tatizo hilo ili kuepusha usumbufu. Mlalamikiwa aliahidi kupeleka huduma ya maji kwa Mlalamikaji haraka iwezekanavyo. Hata hivyo, siku ishirini na moja (21) zilipita na Mlalamikiwa hakuleta utetezi wake kama alivyotakiwa hivyo shauri lilipelekwa kwenye Divisheni kwa ajili ya usikilizwaji wa kesi kama taratibu zinavyotaka. Mnamo tarehe 17 Januari 2025, Mlalamikaji alituma ujumbe kwa Afisa Mtoa Huduma kwa wateja wa EWURA kupitia namba 0688 315223 na kuitarifu Mamlaka kwamba tayari amesharejeshewa huduma ya maji na Mlalamikiwa toka mwezi Desemba 2024 hivyo hana nia ya kuendelea na shauri hili. Mlalamikaji ameishukuru EWURA kwa msaada waliompatia na kuomba kuondoa shauri lake.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yaondolewe na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 14 mwezi Februari 2025.

..........................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**